# HOTUBA YA JAJI MKUU PROF. IBRAHIM HAMIS JUMA

## SIKU YA SHERIA NCHINI, DODOMA

## TAREHE 2 FEBRUARI, 2022

## MAUDHUI: ZAMA ZA MAPINDUZI YA NNE YA VIWANDA: SAFARI YA MABORESHO KUELEKEA MAHAKAMA MTANDAO

---

**Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,**

**Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,**

**Wahe. Majaji wa Mahakama ya Rufani,**

**Mhe. Khamis Ramadhan Abdalla, Kaimu Jaji Mkuu wa Zanzibar,**

**Mhe. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi,**

**Mhe. George B.M Simbachawene (Mb) Waziri wa Katiba na Sheria,**

**Wahe. Majaji wa Mahakama Kuu,**

**Wahe. Majaji Wakuu wastaafu na Majaji Wastaafu,**

**Mhe. Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali,**

**Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania,**

**Mhe. Wilbert Chuma Msajili Mkuu wa Mahakama Tanzania**

**Wakuu wa vyombo vya Ulinzi na Usalama,**

**Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika,**

**Wahe. Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa,**

**Wasajili, Wakurugenzi na Watendaji wa Mahakama,**

**Mahakimu na Mawakili,**

**Viongozi wa vyama vya Siasa,**

**Viongozi wa Dini,**

**Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana.**

**UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Rais,** Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kutujalia amani, afya njema na kwa kutukutanisha kwa mara nyingine tena katika siku hii muhimu kwa Mahakama ya Tanzania. Kwa niaba ya Mahakama ya Tanzania natoa shukrani za dhati kwako kwa kukubali mwaliko wangu wa kuwa Mgeni Rasmi katika sherehe hii. Hii ni mara yako ya kwanza kuadhimisha nasi Siku ya Sheria nchini baada ya kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mnamo tarehe 19 Machi, 2021.

**Mheshimiwa Rais**, Pamoja na kuashiria kuanza kwa Kalenda ya Shughuli za Mahakama, SIKU YA SHERIA ni siku ya kutafakari namna SHERIA ilivyoweza kutuwezesha sisi watanzania, kwa miaka sitini ya uhuru, kuishi pamoja na kufanya shughuli zetu kwa udugu, utulivu, amani na umoja. Hapana shaka yoyote, mfumo wetu wa Sheria na Mahakama, umechangia sisi kuwa wamoja.

Huko Marekani, Siku ya Sheria husherehekewa tarehe Mosi ya Mwezi Mei kila mwaka. Wamarekani hutumia SIKU YA SHERIA kukumbushana umuhimu wa UTAWALA WA SHERIA, na Sheria kama MSINGI wa Taifa lao. Hapa Tanzania, tumejiwekea utaratibu kila mwaka, kabla ya Mwaka wa Mahakama kuanza, MAHAKAMA, WADAU WA SEKTA YA SHERIA wajumuike pamoja na wananchi kukumbushana umuhimu wa Sheria kupitia sherehe ya WIKI YA SHERIA na SIKU YA SHERIA.

**KAULI MBIU MWAKA 2022**

**Mheshimiwa Rais**, kauli mbiu ya Siku ya Sheria mwaka huu ni: - **“ZAMA ZA MAPINDUZI YA NNE YA VIWANDA: SAFARI YA MABORESHO KUELEKEA MAHAKAMA MTANDAO.”** Kauli mbiu hii inatambua MSINGI IMARA wa uwekezaji katika matumizi ya teknolojia na kutekeleza kwa vitendo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Kauli mbiu inatambua pia umuhimu wa kujenga juu ya MSINGI IMARA WA TEKNLOJIA ILIYOPO kwa kutumia Mapinduzi ya Nne ya Viwanda kuleta maboresho makubwa zaidi katika utoaji haki.

**Mheshimiwa Rais**, Miaka 22 iliyopita, Hayati Benjamin William Mkapa (Rais wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) aliandika Utangulizi wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 akiwahadharisha Watanzania kuwa Karne ya **21** iliyoanza tarehe 1 Januari 2000, ilikuwa ikiashiria kuanza kwa dunia iliyo tofauti kabisa na dunia ambayo ilikuwa tumeizoea katika karne ya **20** ambayo ilifikia ukingoni tarehe 31 Desemba 1999. Alituasa tujitayarishe kukabiliana na ushindani mkali utakaokuwa ndio sifa kubwa ya karne ya **21**.

Kwamba, Karne ya 21 itatawaliwa na wale walio na teknolojia iliyo bora zaidi ya wengine, wanaozalisha mali na huduma zenye tija kubwa zaidi ya wengine, wenye miundombinu ya kisasa na bora ya usafiri na mawasiliano, na wenye ujuzi wa hali ya juu, na wenye udhubutu. Alimalizia utangulizi kwa kusema kuwa, kama tunataka, kama taifa, kuwa washiriki hai katika maendeleo ya karne ya 21, lazima tutafute namna ya kuboresha na kujiimarisha katika maeneo yote ya ushindani aliyoyataja.

Kauli Mbiu ya Mwaka huu (2022) inajenga hoja kuwa, Mahakama, wadau wa Mahakama na wananchi kwa ujumla, tujiimarishe zaidi kwa udhubutu wa kutumia teknolojia inayoletwa na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda. Mfumo wetu wa utoaji haki utatoa huduma bora zaidi tukitumia teknolojia zinazozalishwa chini ya Mapinduzi ya Nne ya Viwanda.

**Mheshimiwa Rais,** Mahakama ya Tanzania itakosa fadhila ikijidai kuwa Mahakama ya Tanzania iliwekeza na kutumia vifaa vya TEHAMA kutokana juhudi za Mahakama peke yake bila kubebwa na uwezeshaji mkubwa uliofanywa na Serikali ya Tanzania. Uwekezaji uliwezekana kupitia Mpango Mkakati 2016-

2021 na Programu ya Maboresho uliotokana na Mkopo wa Benki ya Dunia kwa Serikali ya Tanzania kwa manufaa ya Mahakama ya Tanzania. Aidha, uwezeshwaji wa Serikali ulipitia pia miundombinu ya Mkongo wa Mawasiliano, Sheria zilizotungwa na Sera ya TEHAMA na ushauri kutoka wataalamu wa SERIKALI MTANDAO umechangia kuifikisha Mahakama katika matumizi makubwa ya teknolojia katika utoaji haki.

**Mheshimiwa Rais,** Kauli Mbiu ya Mwaka huu ina msisitizo muhimu kuwa, katika kipindi cha miaka minne ijayo kabla ya mwisho wa robo ya kwanza ya karne ya 21 ifikapo 31/12/2025, huduma za Mahakama ya Tanzania zifikie kiwango cha MAHAKAMA MTANDAO. Azma hii itawezekana kwa msingi uliowekwa na utekelezwaji wa Mpango Mkakati wa Mahakama wa Miaka Mitano 2015/16—2019/2020 na Mpango wa Maboresho ya Mahakama, ambao uliongozwa na nguzo tatu za kimaboresho:

1. Utawala Bora, Uwajibikaji na Usimimizi wa Rasilmali;
2. Haki kufikika na kupatikana kwa wakati; na
3. Kuimarisha Imani ya umma kwa Mahakama, na kuwashirikisha wadau.

**Mheshimiwa Rais,** Kauli Mbiu inatutaka tusirudi nyuma katika teknolojia tuliyonayo. Tutumie Mapinduzi ya Nne ya Viwanda kwa kuiendeleza zaidi. Kwa miaka iliyobaki kabla ya tarehe 31/12/2025, ninawasihi watumishi wa Mahakama na wadau wote katika sekta ya Sheria, tuendelee kuvuna faida ya uwekezaji katika teknolojia.

Zipo faida nyingi kutokana na kujenga juu ya msingi wa mafanikio yaliyopo. Uvumbuzi, ubunifu na teknolojia zinaweza kupanua na kufungua mipaka na kuwezesha upatikanaji wa haki kupitia Mahakama zinazotoa huduma kimtandao, msaada wa kisheria na elimu ya sheria kwa umma kupatikana kupitia mitandao, na wananchi wenye matatizo ya kisheria kuweza kupata majibu ya maswali yao kupitia mitandao ili waweze kufanya uamuzi wenye uelewa kabla ya kufungua shauri mahakamani au kutafuta suluhu nje ya Mahakama. Teknojia ndio jibu kwa kuhakikisha kuwa kila mwananchi anapata taarifa muhimu kuhusu upatikanaji wa haki zake. Kwa mfano, teknolojia zinawawezesha wananchi kusoma sheria, taratibu za kimahakama zilizopo katika mitandao na hili huwawezesha hata wale walio mbali na huduma za wanasheria kuweza kujisomea wenyewe sheria hizo na hukumu.

Maboresho yanayoletwa kupitia teknoljia yanayorahisisha upatikanaji wa Haki kwa kila mtu, yana faida ya kusogezea huduma za utoaji haki kuyafikia makundi ya wasiojiweza, ambayo kwa kawaida huwa mbali na huduma za kisheria na utoaji haki. Kwa njia hii, haki itapatikana kwa mizani ya usawa.

**Faida ya Teknolojia kwa Mahakama ya Tanzania**

**Mheshimiwa Rais,** kama nilivyotamka awali, matumizi ya teknolojia Mahakamani kwa kiasi kikubwa sana yamechangiwa uwekezaji mkubwa uliofanya na Serikali katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Teknolojia. Ni baada ya uwekezaji huo, na baada ya kutungwa Sheria na Kanuni wezeshi, Mahakama ya Tanzania imeweza kuanza safari ya kuelekea Mahakama Mtandao

kwa lengo kuu la kuleta ufanisi, uwazi na kuwapunguzia gharama wananchi na watumiaji wengine wa huduma za utoaji haki.

**Mheshimiwa Rais,** uwekezaji uliofanywa na Serikali ya Tanzania katika Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa, umewezesha Mahakama kuunganishwa vituo zaidi ya **157** vya Mahakama kwenye Mkongo huo. Kunganishwa huku umepanua matumizi ya Tehama katika ngazi zote za Mahakama za Tanzania na imewezesha upatikanaji wa haki kwa wakati. Kupitia Mkongo, Mahakama ya Tanzania imesogeza huduma za Mahakama karibu zaidi na wananchi. Aidha, mifumo ya kielektroniki imeweka mazingira ambayo yamewezesha kubadilishana taarifa kati ya Mahakama, taasisi na wadau katika Mfumo mzima wa utoaji haki nchini.

**Mheshimiwa Rais,** moja ya mafanikio makubwa ya matumizi ya TEHAMA katika shughuli za utoaji haki ni Mfumo wa Kielekitroniki wa Kusajili na Kuratibu Mashauri (JSDS2) uliozinduliwa mwaka 2019. Mfumo huu umewezesha na kurahisisha usajili wa mashauri *(Case Registration)*, Majaji na Mahakimu Wafawidhi kuwapangia Majaji na Mahakimu mashauri ya kusikiliza *(Case Assignment)*, utayarishaji wa kumbukumbu za mashauri kuanzia yanaposajiliwa hadi hatua ya kutolewa hukumu au maamuzi *(Case Proceedings),* usajili wa mashauri kwa njia ya mtandao unaowawezesha wadaawa na wadau walio mbali na vituo vya mahakama kusajili mashauri, nyaraka na viambatishi wakati wowote ule, kusambaza taarifa za mashauri kwa wahusika kupitia ujumbe mfupi *(SMS Notification)*.

**Mheshimiwa Rais,** Mfumo wa JSDS2 umeunganishwa na mfumo wa malipo wa Serikali (GePG) kuwezesha kulipa tozo, ada

na faini kwa njia ya mitandao. Ukusanyaji wa takwimu za mashauri umefanikishwa na mfumo wa JSDS2 na taarifa zote za mashauri zinazohitajika hupakuliwa kutoka katika mfumo huu. Dashibodi ya mfumo huu, ni muhimu kwa kutoa taarifa za kitakwimu za kila siku na kila mwezi juu ya mashauri yaliyofunguliwa katika kituo chochote cha Mahakama au ngazi yoyote kuhusu: mashauri yaliyosajiliwa kwa njia za kawaida au kwa mitandao; mashauri yaliyotolewa maamuzi; mashauri ambayo bado yanaendelea; mashauri ambayo hayajapangwa kwa Majaji au Mahakimu; mashauri ya mlundikano; mzigo wa mashauri unaobebwa na kila Jaji au Hakimu. Usimamizi na ufuatiliaji *(Monitoring & Evaluation)* wa shughuli za Mahakama umeimarika sana kulinganisha na kipindi cha nyuma kabla ya uwekezaji huu muhimu.

**Mheshimiwa Rais,** uwekezaji katika TEHAMA umeiwezesha Mahakama kuwa na mfumo wa Usajili, Usimamizi na Utambuzi wa Mawakili *(Mjue Wakili Wako - eWakili),* Mfumo huu unawapambanua Mawakili wenye leseni hai na kustahili kutoa huduma za Uwakili. Huduma nyingine ni upatikanaji wa Maamuzi yote ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani kwa kupitia mfumo wa *TANZLII*, Tovuti ya Mahakama yenye taarifa muhimu kwa wadau, wadaawa, watumiaji wa huduma za Mahakama na wananchi wengine kwa ujumla.

*Virtual Court (Video-Conference)* ni Mfumo wa kutekeleza majukumu mbalimbali yanayohusisha vikao kwa njia ya video bila wahusika kulazimika kukutana ana kwa ana. Mahakama ya Tanzania inatumia Teknolojia hii kuendesha mashauri na kutoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi na wadau wengine. Mfumo

huu umesimikwa katika vituo vya Mahakama na pia katika baadhi ya magereza. Kwa mwaka 2021 pekee, jumla ya mashauri **17,979** yalisikilizwa kwa kutumia mfumo huu. Matumizi ya *virtual court* yanakadiriwa kuokoa kiasi cha shilingi **2,750,092,736** kwa mwaka kwa upande wa Magereza, Mawakili, Mahakama na Wadau wengine.

**Mheshimiwa Rais,**

Nafurahi pia kukujulisha wewe na umma wa watanzania kuwa kuanzia tarehe 01 Septemba, 2021 MAHAKAMA inatumia Ofisi Mtandao *(e-office)* kuendesha shughuli za kiutawala. Mfumo huu unaendeshwa na kusimamiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) chini ya Ofisi ya Rais Utumishi. Matumizi ya mfumo huu yanaokoa gharama kubwa ya shajala *(stationeries)* na muda wa kushughulikia majalada. Mfumo huu uwawezesha Viongozi wa Mahakama kushughulikia majalada mahali popote wanakapokuwa maadamu kuna *Internet* pamoja na program maalum ya "*Virtual Private Network (VPN)*" ambayo inaunganisha mtumiaji na mtandao wa Serikali (GovNet). Mfumo huu unatunza siri kuliko hata nakala ngumu.

**Mheshimiwa Rais,**

Kwenye hili la *e-office*, naomba kutoa wito kwa wadau wetu wote kwamba hawana haja tena ya kuhangaika kutuma barua kwa posta au kuleta Makao Makuu ya Mahakama Tanzania, badala yake tunayo masijala ya Makao Makuu kwenye mtandao na kwamba baada ya kuweka barua kwenye mfumo wa pdf, kwa barua za kawaida tuma kama kiambatisho kwenye anwani ya barua pepe ambayo ni; barua@judiciary.go.tz na kama ni barua ya

siri tuma kwenye baruasiri@judiciary.go.tz . Kwa kufanya hivyo mteja atakuwa amekabidhi barua yake kwenye masijala yetu na hana haja tena ya kutuma nakala ngumu. Mara barua yake itakapopokelewa atajulishwa muda uleule kwa njia ya Barua Pepe kwamba tumeipokea na inashughulikiwa. Bado wadau hawajabadilika kifikra kwani wengi kwenye taasisi nyingi bado wanatuma nakala ngumu kisha tuanze tena kuzibadili kutoka nakala ngumu na kwenda nakala tepe ili kufanyiwa kazi kwenye *e-office*.

**Mheshimiwa Rais,**

Kwa kuonyesha dhamira ya dhati ya kuelekea Mahakama Mtandao, Mahakama imenunua ***laptop* 1,388** kwa Majaji na Mahakimu. *Laptop* hizi ni nyenzo muhimu katika kutelekeza majukumu yao katika mazingira ya mahakama mtandao. Pamoja na kutumia laptop hizi kuandika hukumu na mwenendo wa mashauri. Vilevile, zinatumika katika kufanya tafiti na hivyo kuongeza ubora wa hukumu na upatikanaji wa haki kwa wakati.

**Mheshimiwa Rais,** Kwa upande wa huduma za internet na mtandao wa ndani (MPLS VPN), Mahakama ilikuwa inatumia jumla ya Shs. **113,473,911.64** kwa mwezi. Hata hivyo, viwango vya "bandwidth" haviendani na mahitaji halisi ya Mahakama; Mhe. Rais wakati wa hotuba yako ya uzinduzi wa Vituo Jumuishi vya Utoaji Haki (IJC) sita tarehe 6 Oktoba 2021, ulielekeza Mtendaji Mkuu wa Mahakama kukutana na viongozi wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na Wizara ya

Fedha na Mipango kushughulikia mahitaji ya Mahakama ya ongezeko la *bandwidth*.

**Mheshimiwa Rais,** Ninafuraha kukutaarifu kuwa utekelezaji wa maelekezo yako unaendelea vizuri na mpaka sasa Mahakama inapata huduma ya "**internet**" ya serikali kupitia Mamlaka ya Serikali Mtando (eGA). Wakati huo huo, IJC-Dodoma na Mahakama Kuu Masijala Kuu zimeingizwa moja kwa moja kwenye Mtandao wa Serikali (GovNet). Hatua hizi zimepunguza gharama za uendeshaji kwa jumla ya Shs. **41,353,053.25** kila mwezi. Ninamshukuru sana Waziri wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Mhe. Nape M. Nnauye) pamoja na watendaji wake na Waziri wa Fedha na Mipango (Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba) na watendaji wake kwa ushirikiano mkubwa ambao wanatupatia katika kutatua changamoto ya *Bandwith.*

**Huduma za Mobile Courts**

Katika kusogeza huduma kwa wananchi, Mahakama imeendelea kutoa huduma za Mahakama inayotembea (Mobile Court) katika maeneo mbalimbali ya Mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza. Lengo la Mahakama ni kuongeza magari mengine **6** ya kutoa huduma ya Mahakama inayotembea. Kwa mwaka 2021 pekee Mahakama inayotembea imesikiliza mashauri **866** kati ya mashauri **963** yaliyopokelewa.

**Hatua hadi kufikia Mahakama Mtandao**

**Mheshimiwa Rais,** safari kufikia Mahakama Mtandao ilianza kwa usanifu na ubunifu wa barabara ya kufikia hiyo Mahakama

Mtandao inayotarajiwa. Chini ya Mradi wa Maboresho yanayofadhiliwa na Benki ya Dunia, Kampuni 5 za kimataifa na 2 za ndani ziliomba zabuni, Kampuni ya TEHAMA ya NET GROUP kutoka Estonia ndio ilishinda zabuni ya kuwa Mtaalamu Elekezi *(Technical Advisor)* kwa kazi ya kutayarisha uchambuzi wa kina *(detailed feasibility study)* kuhusu mahitaji, utayari na matumizi ya TEHAMA katika Mahakama ya Tanzania, katika safari yake kuelekea Mahakama Mtandao. Katika kupendekeza hatua za kutekelezwa ili kufikia hiyo Mahakama Mtandao, Kampuni ya NETGROUP ilitakiwa kuendeleza mafanikio yaliyopatikana kutoka katika Mfumo wa kielektroniki wa Kusajili na Kuratibu Uendeshaji wa Mashauri (JSDS2).

**Mheshimiwa Rais,** Kwa mujibu wa Mtaalamu Elekezi, matayarisho ya Mahakama Mtandao ni pamoja na matayarisho ya kuhama kutoka kupunguza matumizi ya karatasi hadi matumizi kwa njia za ki-elektroniki *(Migration of records from paper to electronic systems)*. Idara ya Usimamizi wa Mashauri ikishirikiana na Idara ya TEHAMA zilishirikiana kuchakata na kuhandisi upya taratibu na hatua zote za kimahakama katika ngazi zote za mahakama ili zisanifiwe na kugeuzwa kutoka utegemezi wa karatasi hadi kuwa taratibu za ki-elektroniki. Zoezi hili linaitwa *"Court Business Process Re-engineering."*

Mtaalamu Elekezi alipewa majukumu kadhaa muhimu. **Mosi**, alitakiwa kuchambua hatua na changamoto zote zitakazoweza kujitokeza katika mpango mzima wa safari ya kutoka ngazi zote za mahakama za kawaida hadi kufikia Mahakama Mtandao. Lengo hapa ni kuboresha ufanisi, kuongeza uwazi katika utoaji haki na

kufikia viwango vya kitaifa na kimataifa vya utoaji haki unaolenga manufaa ya wananchi *(citizen-centric justice delivery)*.

**Pili,** Mtaalamu Elekezi alipewa pia jukumu la kupima utayari wa Mahakama ya Tanzania kuhama *(Digital Migration)*, na mambo ya kufanywa wakati wa mpito kutoka Mahakama za Kawaida (*Manual*) hadi mahakama mtandao endelevu; kuboresha usalama wa taratibu na mipangilio ya kimahakama katika utoaji haki; usalama wa nyaraka za kimahakama; Menejimenti ya Mashauri*;* ufanisi wa upatikanaji wa taarifa za Mahakama na za kimahakama*.*

**Tatu,** alitakiwa aainishe hatua zote ambazo mashauri mbalimbali na shughuli za kimahakama hupitia hadi haki kutolewa kwa wahusika. Maainisho haya ni matayarisho ya kuhamisha hatua hizi kwenda kuwa hatua za kimtandao. Baada ya kuhama, hatua za kimtandao zitahusu usimamizi wa mashauri kwa njia ya mtandao, huduma na nyaraka pepe za kimahakama, usajili wa mashauri kwa njia ya mtandao, hukumu pepe, utafiti kufanyika kupitia Maktaba Mtandao, na kadhalika**.**

**Nne,** baada ya kuzipitia taratibu za shughuli za kimahakama *(court business processes)* Mtaalamu Elekezi alipewa jukumu la kubuni na kusanifu mfumo wa kimtandao ambao utaendesha shughuli zote za kimahakama na kuunganisha na shughuli za wadau wote wa Mahakama.

Mtaalamu Elekezi alieleza kuwa safari ya Mahakama Mtandao itahusu kukamilika kwa mifumo sita au zaidi ya matumizi ya TEHAMA, ambayo ni: (i)-Mfumo wa Usimamizi wa Mashauri Mahakamani *(Case Management)*; (ii)-Mfumo wa Utawala Ki-elektroniki *(e-Administration)*; (iii)-Mfumo wa Kushughulikia

Malalamiko Ki-elektroniki *(e-Complaints)*; (iv)-Mfumo wa Usimamizi wa Hati na Nyaraka Ki-elektroniki *(e-Document Management)*; (v)-Maktaba-Mtandao (e-*Library*) na (vi)-Usimamizi wa Mali Ki-elektroniki *(e-Asset Management).*

**Mheshimiwa Rais,** Historia inatufundisha kuwa kazi ya kuhama kutoka mfumo mmoja hadi mwingine sio nyepesi; ikizingatiwa kuwa kuhama kunahusisha pia mabadiliko ya kifikra na kiutendaji kazi *(Change of attitudes and work culture)*. Kazi ya Mtaalamu Elekezi ni nyepesi kuliko kazi ya utekelezaji ambao watumishi wa Mahakama na Wadau wanawajibika kutekeleza na kufikia Mahakama Mtandao. Kazi muhimu ya awali ni ile ambayo Mtaalamu Elekezi aliita *"Business Process Re-Engineering."* Kwa Mahakama, hii ina maana ni kupitia upya mnyororo mzima wa utoaji haki kuanzia shauri linapofunguliwa, kupangiwa Jaji au Hakimu, kupitia hatua zote za kusikilizwa kwa mujibu wa ngazi mbali mbali za mahakama hadi kufikia uamuzi wa mahakama; kutathmini zitahamiaje kuwa taratibu za kimtandandao zinazobeba ufanisi, uwazi na uharaka wa utoaji haki. Kwa kuwa mnyororo mzima wa utoaji haki unaongozwa na taratibu za kisheria, uhamiaji kwenda katika Mahakama Mtandao utahitaji mabadiliko ya sheria na taratibu za kimahakama hususan mabadiliko yanayopunguza vituo katika mnyororo, kwa nia ya kuweka ufanisi na uwazi katika utoaji haki. *Business Process-Re-engineering* ni kutazama upya kabisa sheria zinazotumika na Mahakama, kutazama upya taratibu na mfumo mzima wa utoaji haki na kuusanifu ili utumike katika mazingira ya mahakama mtandao kwa nia ya kuongeza ufanisi katika utoaji haki, kwa ubora, haraka zaidi na kwa gharama nafuu.

Upembuzi uliofanywa na Mtaalamu Elekezi ulibaini mambo kadhaa ambayo ni muhimu katika kufanikisha safari ya Mahakama Mtandao.

**MABADILIKO YA KIFIKRA NA KIUTENDAJI KAZI NI KUTUMIA SERA, SHERIA, TARATIBU NA UWEZESHWAJI ULIOPO KUFIKISHA MAHAKAMA NA WADAU KATIKA MAHAKAMA MTANDAO**

**Mheshimiwa Rais,** Mahakama Mtandao itajengwa katika msingi wa mafanikio yalipo na yajayo. Mahakama itaendelea kutegemea Uwekezaji utakaokuwa ukifanywa na Serikali kadri teknolojia itakavyokuwa ikibadilika kulingana na kasi ya Mapinduzi ya Nne ya Viwanda.

Aidha, Mahakama imefanikiwa kuwekeza katika TEHAMA kutokana na Sheria na Kanuni kama Sheria ya Shughuli za Kimtandao ya Mwaka 2015 (*Electronic Transactions Act 2015—Act 13 Of 2015*), zilizotungwa kuweka mazingira mazuri ya matumizi ya TEHAMA. Hivyo hivyo, mafanikio ya Mahakama Mtandao yatategemea mabadiliko ya sheria na kanuni kadri Mapinduzi ya Nne yatakavyokuwa yakileta mabadiliko katika teknolojia. Nimeeleza awali kuwa matumizi ya TEHAMA katika shughuli za kimahakama yamewezekana kupitia Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Mtaalamu Elekezi aliitaarifu Mahakama kuwa mfumo wa kisheria uliopo Tanzania unaweza kuhimili na kulea Mahakama Mtandao.

**Vitambulisho vya Taifa na Anwani za Makazi ni Wezeshi kwa Mahakama Mtandao**

Safari ya Mahakama Mtandao itawezeshwa pia na Mfumo wa Vitambulisho vya Taifa. Safari itategemea sana Mfumo wa Anwani za Makazi ambao umetolewa na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha, mfumo wa POSTIKODI chini ya Wizara ya Mawasiliano utaisadia Mahakama katika kujenga mfumo wa Mahakama Mtandao.

Katika kikao cha Bajeti cha mwaka jana (2021), Waziri anayesimamia TEHAMA alibainisha umuhimu wa Mradi wa Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi. Mhe Waziri Dkt. Ndugulile alisema: *"Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi ni Mradi unaotoa taarifa sahihi ya anapopatikana mwananchi na utambulisho wa matumizi ya eneo husika. Taarifa hizo zinarahisisha utoaji na ufikishaji wa huduma za Serikali na kijamii mahali alipo mwananchi sambamba na kuwezesha biashara mtandao (e-Commerce)."* Hii mradi ni muhimu pia kwa Mahakama inayoelekea kuwa na Mahakama Mtandao. Kunapokuwa na biashara mtandao, lazima pia kuwepo kwa mfumo wa kutatua migogoro ya kibiashara kwa njia ya mtandao *(online dispute resolution)*. Aidha, mashauri yanapofunguliwa Mahakamani, husajili majina ya wahusika (washtakiwa, wadaawa) na baadaye hata Mashahidi. Anuani za makazi za watu hawa ni muhimu sana katika ubora wa huduma za Mahakama, hasa inayosajili mashauri kwa njia ya Mtandao. Mahakama inapenda kuwa kila Mtanzania ambaye anayo kadi ya uraia, aweze kujidhamini pale anaposhtakiwa kwa makosa yanayodhaminika. Mahakama haitaweza kutoa dhamana kwa wepesi pale kadi ya uraia haiambatani na uthibitisho wa anuani ya Makazi ya muhusika.

**MKONGO WA TAIFA UNAUNGANISHA MIFUMO, TAASISI ILI IWEZE KUZUNGUMZA NA KUSOMANA**

Uwepo wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano *(ICT broadband Back-Borne)* ni muhimu katika kuviunganisha vituo mbali mbali vya Mahakama, na kuunganisha Mahakama na wadau wake na watumiaji wa huduma za Mahakama Mtandao kwa ujumla.

**Mheshimiwa Rais,** sasa ndio wakati wa Taasisi za umma ambazo zimefanya uwekezaji mkubwa katika mifumo ya teknolojia kuunganishwa na mifumo kuweza kusomana kupitia Mapinduzi ya Nne ya Viwanda.

Kwa mfano, mifumo ya kidijitali kuhusu miliki na matumizi ya ardhi inayosimamiwa na Wizara ya Ardhi, ziweze kusomeka na kutumiwa moja kwa moja na Mahakama za Ardhi, Mabenki, wawekezaji na hata wafanya biashara bila kutembelea masjala za ardhi. Urahisi wa kufahamu historia ya ardhi anayotaka kufanyia shughuli za kiuchumi ni muhimu katika migogoro inayopoteza muda wa kusikilizwa Mahakamani. Mfumo wa kidijitali kuhusu miliki na matumizi ya ardhi inayosimamiwa na Wizara ya Ardhi isijikite tu katika kukusanya Kodi ya Ardhi na Kodi ya Majengo peke yake; mfumo usaidie kusoma na taasisi zingine kwa faida ya kupunguza migogoro inayoletwa katika ngazi mbali mbali za Mahakama za Ardhi na itumike pia kufanikisha shughuli za kiuchumi.

**AKILIBANDIA/AKILI TARAKILISHI YA MAPINDUZI YA NNE YA VIWANDA INATULAZIMU KUBORESHA NAMNA TUNAVYOTUMIA TEKNOLOJIA TULIYOWEKEZA**

**Mheshimiwa Rais**, Kuongezeka hivi karibuni kwa matumizi ya Akili Bandia/Akili Tarakilishi *(Artificial Intelligence - AI)* katika ufanyaji kazi maofisini na hata uzalishaji viwandani ni matokeo ya zama za Mapinduzi ya Nne ya Viwanda. Mapinduzi ya Nne ya Viwanda yanatulazimu sote tubadili namna ya kutumia teknolojia tulizowekeza pamoja na kubadili mitizamo katika kiutendaji kazi, utoaji huduma kwa umma, uzalishaji uchumi, na kiuwekezaji. Mapinduzi ya Nne ya Viwanda yanazitaka Taasisi za Umma na Taasisi binafsi zihakikishe kuwa mifumo yao ya teknolojia inawasiliana na inaongea katika kufanikisha ufanisi na uwazi katika utoaji wa huduma kwa umma.

**MFANO WA MFUMO WA DIJITALI WA KUSIMAMIA REKODI ZA ARDHI UZUNGUMZE NA KUSOMANA NA MASJALA ZA MAHAKAMA KUPUNGUZA MIGOGORO YA ARDHI**

Mfano wa karibu wa mifumo mbali mbali ya teknolojia ya Taasisi kusomana na kusaidiana katika dunia ya Mapinduzi ya Nne ya Viwanda ni ule wa jirani yetu Jamhuri ya Kenya. Mafanikio yanayotarajiwa kutoka katika utekelezaji wa mfumo wa dijitali wa kusimamia rekodi za ardhi uitwao ARDHISASA uliozinduliwa na Rais Uhuru Muigai Kenyatta mwezi Aprili mwaka jana (2021) ni kupunguza mashauri ya ardhi yanayowasilishwa mahakamani. *Blog* ya China Radio International imeuelezea mfumo wa ARDHISASA:

> *"Mfumo huo unaofahamika kama "ArdhiSasa" utakuwa na rekodi zote za ardhi nchini Kenya , ambapo wananchi wataweza kutafuta habari za umiliki wa ardhi, kutuma maombi ya hati miliki, kuuza ardhi na shughuli zingine za mashamba.*
>
> *Kuzinduliwa kwa mpango huo kutashirikisha na kutoa suluhisho kwa mizozo ya kihistoria ya ardhi*

*pamoja na kutoa hakikisho la usalama na thamani ya hati yako ya umiliki wa ardhi na hivyo kuzingatia wito wa 'Shamba Lako, Hati Safi.*

*Kufuatia uzinduzi wa "Ardhisasa", mfumo wa zamani wa usimamizi wa ardhi jijini Nairobi umeondolewa. Hata hivyo, wamiliki wa ardhi ambao huenda wakose kupata hati zao wanashauriwa kuwa wavumilivu huku Wizara ya Ardhi inapoendelea kuimarisha jukwaa hilo la kidijitali. Waziri wa Ardhi Faridah Karoney alisema jukwaa hilo la kidijitali litatumika kama kituo cha kutoa huduma na taarifa zote za Serikali kuhusu masuala ya ardhi.*

*Katibu wa Wizara ya Ardhi, Nicholas Muraguri alisema jukwaa la Ardhisasa litawawezesha Wakenya kuanzisha na kufuatilia shughuli za mashamba wakiwa nyumbani au ofisini kwa kutumia simu au tarakilishi."*

*http://swahili.cri.cn/20210428/6ac7b0c4-8225-c64a-3247-f788cee3ca36.html*

**Mheshimiwa Rais**, hapana shaka yoyote kuwa, Mapinduzi ya Nne ya Viwanda yanachukua fursa nyingi ambazo hapo awali zilikuwa zikishikiliwa na binadamu. Hata hivyo, mapinduzi hayo, kwa mfano matumizi ya roboti inayofanya kazi kama mwanadamu, italeta faida kubwa ya kuongeza ufanisi.

**Mheshimiwa Rais,** ili tuweze kuyafaidi Mapinduzi ya Nne ya Viwanda Pamoja na Akili bandia/Akili Tarakilishi *(Artificial*

*Intelligence)*, hatuna budi kuyafahamu na kutambua maeneo ambayo yametumika na kutoa faida.

Akili Bandia / Akili Tarakilishi (AI) inaweza kuelezewa kuwa ni kuruhusu mashine kuwa na tabia ambayo inaweza kutafsiriwa kuwa ni ya kutumia akili kama binadamu ambaye angeweza kuwa na tabia hiyo iliyooneshwa na mashine. Hii ndio tafsiri ambayo bwana mmoja aitwaye John McCarthy aliitumia mwaka 1956 alipozungumzia *Artificial Intelligence*. Akili Bandia / Akili Tarakilishi imetafsiriwa pia kuwa ni uwezo wa mashine kuiga akili za binadamu na kufanya kazi kama kutatua tatizo, kufikiri, kugundua na kutafuta maana, kutabiri jambo au, kujifunza kutokana na uzoefu uliopita. Akili Bandia /Akili Tarakilishi ni kuifundisha mashine ifikiri na kutoa maamuzi chini ya uangalizi au hata bila ya uangalizi, na hujumuisha pia kutumia lugha zaidi ya moja. Ili Akili Bandia au Akili Tarakilishi iweze kufanya kazi, inahitaji ukusanyaji wa taarifa za kutosha (*big data*). Akili Bandia inajitokeza katika mifumo au aina mbali mbali, kwa mfano, utambuzi wa hotuba/sauti au utambuzi wa sura au picha *(speech recognition, face or image recognition).*

**MAHAKAMA YA TANZANIA YATAFUTA AKILI BANDIA KWA AJILI YA KUTAFSIRI NA KUANDIKA TAARIFA ZA MASHAURI MAHAKAMANI KWA LUGHA YA KISWAHILI**

**Mheshimiwa Rais,** uundaji wa Roboti ambazo zinafanya baadhi ya shughuli za Wanasheria, ni ujumbe tosha kwa tasnia ya sheria juu ya kujiimarisha kwa kujiendeleza zaidi ili kukabiliana na ushindani mkubwa unaoendelea kufuatia mapinduzi ya nne ya viwanda. Kutokana na mabadiliko haya kwenye matumizi ya TEHAMA, Mahakama inafanya jitihada za dhati ili kupitia

matumizi ya *Artificial Inteligence (AI)*, tuwe na mfumo wa kutafsiri na kuandika taarifa za mashauri mahakamani kwenye lugha zaidi ya Kumi. Mkakati huu uko kwenye hatua nzuri ya majadiliano. Faraja kubwa tuliyonayo ni kwamba katika maandalizi ya Programu hii, hati-miliki ya modeli ya Kiswahili *(Swahili Language Model)* itakuwa chini ya Mahakama ya Tanzaniag ili Mahakama zingine duniani zikitaka kutumia, lazima wapate kibali cha Mahakama ya Tanzania na walipe *'license fee'* ambayo itakuwa ni chanzo cha mapato kwa Serikali. Kwa mantiki hii tunaweka dhana ya Serikali **'kubidhaisha Kiswahili'** kwenye vitendo. Tutashirikiana kwa karibu na Wizara yenye dhamana na Kiswahili ili kuzidi kuimarisha matumizi ya Kiswahili katika Mahakama za Afrika Mashariki (EAC), SADC na maeneo mengine.

**Mheshimiwa Rais,** Programu hii tarajiwa ya kutafsiri kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili ni kutambua ukweli wa maneno ya Rais wa Awamu ya Tatu Hayati Benjamin William Mkapa kuwa, Karne ya 21 itatawaliwa na wale walio na teknolojia iliyo bora zaidi ya wengine.

**Mheshimiwa Rais,** uamuzi wa Mahakama kutumia teknolojia na kuvuna faida kutoka katika Mapinduzi ya Nne ya Viwanda, ni kuhakikisha kuwa Nchi yetu inapojenga uchumi shindani, utoaji wa haki unakuwa wa viwango vinavyokidhi huo ushindani. Mahakama ya Tanzania haiwezi kufumbia macho yale yanayoendelea katika jamii wala kubaki nyuma au kuendelea kukumbatia mifumo ya kizamani ya uandishi wa mienendo ya mahakama kwa kuandika kwa mikono wakati Akili Bandia ipo kuweza kufanya kazi hiyo kwa wepesi na bila gharama. Mahakama

ya Tanzania haiwezi kubaki katika zama za kianolojia *(analog system)* iliyopitwa na wakati katika mfumo la utoaji haki.

**KARNE YA 21 NI WAKATI TANZANIA IFIKIRIE ONLINE COURTS**

**Mheshimiwa Rais,** Katika muda huu kabla ya mwisho wa robo ya kwanza ya Karne hii ya 21, ndio wakati sahihi kwa Mahakama ya Tanzania, kwa kushirikiana na Mihimili ya Serikali na Bunge; kuanzisha mifumo ya kimahakama ya kidijitali kwa ajili ya utatuzi wa migogoro ya kibiashara inayofanyika kidijitali.

Kama ambavyo biashara za kawaida zinazofanyika nje ya mitandao huzua migogoro inayohitaji usuluhishi, hivyo hivyo, biashara kupitia mitandao inahitaji mifumo ya kusuluhisha migogoro kwa haraka na ufanisi *(expedited Online Dispute Resolution)*. Mamlaka za Tanzania zinatakiwa kuweka mifumo ya kimtandao, ambayo itawahakikishia wanaofanya biashara kupitia mitandao, wafanye biashara wakijua kuwa kuna mifumo ya utatuzi wa migogoro na hii itakuza biashara za ndani na nje ya Tanzania kupitia mitandao.

Profesa Richard Susskind, alikuwa Mshauri Maalum wa Jaji Mkuu wa Uingereza kuhusu maswala ya matumizi ya Teknolojia katika utoaji wa haki. Amekuwa Mshauri kwa Majaji Wakuu Sita wa Uingereza (Thomas Henry Bingham; Harry Kenneth Woolf; Nick Phillips; John Thomas; na Ian Duncan Bunnet). Mwezi Septemba Mwaka jana (2021), alitoa Mada Maalum katika Mkutano wa Mwaka wa Jukwaa la Majaji Wakuu wa Nchi za Kusini na Mashariki ya Africa *(Southern Africa Chief Justices Forum*). Pamoja na kutoa mada, aliwapa Majaji Wakuu nakala ya kitabu chake

alichokiandika mwaka 2019, kiitwacho— “ONLINE COURTS AND THE FUTURE OF JUSTICE!” Yeye ni muumini mkubwa wa huduma za usikilizwaji wa mashauri kufanyika kupitia mitandao bila wahusika wote kukusanyika katika jengo moja (*ONLINE COURTS*).

*ONLINE COURTS* ni mahakama ambayo Majaji, Mahakimu, Waendesha Mashtaka, Mawakili, Washtakiwa, Mashahidi na waadaawa hufanya kazi zao zote au sehemu za kazi zao za utoaji huduma za haki kupitia mitandao badala ya kukusanyika katika kumbi za mahakama kama tulivyozoea.

Profesa Richard Susskind aliwasihi Majaji Wakuu wachangamkie faida lukuki zitokanazo na matumizi ya ONLINE COURTS. Alitaja baadhi ya faida kuwa ni zaidi ya maamuzi (hukumu) kupatikana kwa urahisi kwa kila mtu. Faida zingine kubwa ni pamoja na kuwawezesha watumiaji wa huduma za mahakama kuelewa sheria zinazotumika kuendesha mashauri yao, kuwewezesha watumiaji kujaza fomu mbali mbali, na kuwewezesha hata kuendesha mashauri yao bila kuwategemea mawakili.

Profesa Richard Susskind aliwasihi watunga sera, Majaji, Wanasheria katika nchi zote kuangalia upya sheria, taratibu na mazoea katika ngazi mbali mbali za mahakama na kupendekeza namna ambavyo mfumo huu ulipo sasa unaweza kuruhusu mfumo wa usikilizaji na utoaji haki kwa njia za mtandao. Aliwasihi kusimama imara dhidi ya changamoto watakazokutana nazo na kuangalia picha kubwa duniani, ambako ushindani katika utoaji haki umefanikishwa sana na matumizi makubwa ya teknolojia. Aidha, amewataka watambue kuwa zaidi ya nusu ya watu duniani

wako mbali na huduma za sheria na utoaji haki changamoto ambayo itapunguzwa kwa kiasi kikubwa na matumizi ya teknolojia.

Profesa Richard Susskind amewasisitizia watunga sera, Majaji, Wanasheria kuwa, tupende tusipende Karne hii ya 21 ni ya Maboresho kupitia Mapinduzi ya Nne ya Viwanda. Ametukumbusha kuziangalia upya SHERIA zetu zote, KANUNI zote na TARATIBU zetu zote za utoaji haki; na tufanye tathmini kama zinakwenda sambamba na kasi ya Mabadiliko Makubwa katika Mapinduzi ya Nne ya Viwanda. Amekumbusha kuwa leo hii, mifumo yetu ya KIMAHAKAMA, SHERIA ZETU, pamoja na TAALUMA NZIMA ZA SHERIA na ELIMU YA SHERIA—zimeganda katika maudhui ya dunia ya karne za 19 na 20, na hazikidhi kabisa kasi, ubora na mahitaji ya wananchi wa Karne ya 21.

**WADAU WA MAHAKAMA WASIACHWE KATIKA SAFARI MAHAKAMA MTANDAO**

**Mheshimiwa Rais**,

Wadau wa Mahakama wanahitaji uwezeshwaji, kama Mahakama ilivyowezeshwa.

Safari ya kuelekea Mahakama mtandao haiwezi kamwe kufikiwa ikiwa wadau wa Mahakama watabaki nyuma. Nichukue fursa hii kuwapongeza wadau wote wa Mahakama ambao

wameanza kuchukua hatua ya kuelekea katika matumizi ya TEHAMA.

Nichukue fursa hii kuwaomba wadau wote wa Mahakama kuchukua hatua za makusudi sio tu kuunga mkono juhudi za Mahakama katika matumizi ya TEHAMA bali nao kutumia TEHAMA katika kutoa huduma zao.

**Mheshimiwa Rais,**

Kama nilivyoeleza awali Mahakama inaufanyia maboresho makubwa mfumo wake wa Menejimenti ya Mashauri (JSDS 2) ili kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia. Mfumo huu mpya utakuwa na hadhi ya *Advanced Case Management*. Pamoja na mambo mengine, mfumo huu hautaruhusu ufunguaji wa mashauri kwa njia ya kawaida, utakuwa na uwezo wa kutengeneza jalada la ki-eletroniki la mashauri (Electronic case file), utawezesha ubadilishanaji wa majalada ya mashauri kwa njia ya ki-eletroniki, kuwekwa saini ya ki-eletroniki kwenye kumbukumbu *(Digital Signature)* n.k. Sambamba na hilo mfumo huu utashuka mpaka ngazi ya Mahakama za mwanzo.

Mategemeo yetu ni kuwa mafanikio ya mikakati yetu hiyo miwili yatatufikisha katika hatua ya kutotumia karatasi (*paperless Court*), mpango ambao tumeuanza kwa majaribio katika Mahakama ya Wilaya Kigamboni na kupata mafanikio na tumejifunza maeneo ya kuboresha.

**Mheshimiwa Rais,** Pamoja na jitihada za Mahakama za kutumia TEHAMA katika utoaji haki, bado zipo sheria nyingi zinazokinzana na matumizi ya TEHAMA katika utoaji haki.

Miongoni mwa sheria hizo ni Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, Sheria ya Ushahidi n.k. Nimeshamuomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwasiliana na uongozi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuangalia uwezekano wa kuzifanyia marekibisho sheria hizi ili ziendane na hali ya sasa.

**Mheshimiwa Rais,** Kwa upande wa Mahakama, tumeshafanya marekebisho ya kanuni kadhaa za Jaji Mkuu na kutunga kanuni mbili yaani Kanuni za Ufunguaji wa Mashauri kwa Njia ya Mtandao *(The Judicature and Application of Laws (Electronic Filing Rules, 2018)* pamoja na Kanuni za Usikilizaji wa Mashauri kwa Njia ya Mtandao *(the Judicature and Application of Laws (Remote Proceedings and Electronic Recording) Rules, 2021).*

**Mheshimiwa Rais,**

Wakati tukijipanga kutoa taarifa muhimu kwa wananchi kupitia teknolojia, Kwa mwaka huu wa 2022, tunategemea kuanzisha Kambi za Mahema ya Haki (Justice Tents Camps) hasa katika maeneo yaliyopo mbali na huduma za Mahakama, na kwamba yatakuwa na utaratibu wa kuwekwa kwa ratiba maalum kutokana na mahitaji na tutakuwa na Mahakimu na Majaji wasiokuwa na mipaka (Borderless Judges and Magistrates - BJM). Tunatambua kuwa kuna makundi ambayo sio rahisi kufikiwa na huduma za Mahakama kutokana na jiografia yao au shughuli zao.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Rais,** Katika zama za mapinduzi ya nne ya viwanda matumizi ya TEHAMA katika utoaji haki hayaepukiki kabisa. Kwa kuwa pia suala la utoaji haki ni mtambuka, wadau wote katika mnyororo wa haki wana jukumu la kuhakikisha TEHAMA inatawala mchakato mzima wa utoaji haki katika hatua zote za shauri. Mahakama tukitembea wenyewe hatutafika mbali.

Mwisho kabisa nikushukuru tena Mhe. Rais kwa kukubali kutenga muda wako kuhudhuria na kuwa mgeni rasmi katika siku hii muhimu. Niwashukuru pia wananchi waliojitokeza kwenye wiki ya elimu ya sheria. Nina imani kubwa kuwa wamejifunza mambo mengi yahusuyo Mahakama na Wadau wake.

**Mheshimiwa Rais,**

Mheshimiwa Rais, sasa nikuombe utufanyie mambo mawili makubwa ambayo wadau wa Sheria na Watanzania kwa ujumla wanasubiri yaani; Kuhutubia hadhara hii ambapo utakuwa anaongea na Taifa kwa ujumla kupitia vyombo vya Habari, na la pili ni kutuzindulia mwaka wa kazi wa kimahakama kwa mwaka 2022,

Mhe. Rais Karibu sana!

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**